HALMASHAURI YA WILAYA YA BUSEGA

SHULE YA SEKONDARI IGALUKILO,
S.L.P 330,
BUSEGA
Barua pepe: christerkalega88@gmail.com
SIMU: 0764328258/ 0782445544
14/12/2020

Kumb. Na. IGSS/F1/2021/ ……..
Jina la mwanafunzi ……..
S.L.P ……..

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI IGALUKILO WILAYA YA BUSEGA MKOA WA SIMIYU.

1.0 UTANGULIZI

Nina furaha kukutaarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha KWANZA katika shule hii mwaka 2021. Shule ya sekondari igalukilo ipo umbali wa Km 25 mashariki mwa makao makuu ya halmashauri ya Busega.

Muhula wa kwanza wa masomo utaanza tarehe 11/01/2021. Unatakiwa kuripoti kuanzia tarehe 11/01/2021 na mwisho wa kuripoti ni tarehe 25/01/2021 ndani ya siku kumi na nne tu (14).

2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

2.1 Sare za shule

A. Wavulana

- Sare ya shule hii ni suruali **NYEUSI** mbili (2) zenye mifuko mitatu, marinda mawili kila upande kwenye mfuko wa mbele, upana wa chini inchi (20-22),

  NB;Modol hairuhusiwi.
- Viatu vyeusi vya ngozi vyenye kamba na soksi nyeusi
- Shati nyeupe mbili mikono mifupi

B. Wasichana

- Shati nyeupe mbili (2) mikono mifupi na sketi ndefu nyeusi mbili (2) zenye rinda box ndefu na marnda ya kupangwa na mfuko mmoja tu. Sketi iwe na belti ya sm 3 kwa 4
- Viatu vyeusi visivyo na kamba (simple shoes)
- Soksi nyeupe fupi

  NB: rangi ya hijabu ifanane na sare ya shule.

C. Sare ya michezo

- Jezi ya bluu yenye kola isiyo na maandishi na suruali **“track”** ya bluu.
- Raba nyeusi au nyeupe.

2.2 VIFAA VYA USAFI

a) **Wavulana**: jembe moja lenye mpini
b) **Wasichana:** ndoo moja ya lita 10 na soft bloom moja.
c) Mfagio wa chelewa (1) kwa kila mwanafunzi (wavulana kwa wasichana)

2.3 VIFAA VYA TAALUMA

a) Madaftari kumi (10) (counter books) kuanzia quire 2.
b) Kalamu za wino za kutosha, kalamu za risasi (pencils) na ufutio.
c) Bofa (mmathematical set) na vifaa vyake vyote.
d) Dictionary kwa ajili ya muongozo wa kujifunza kiingereza (ni lazima mwanafunzi anaporipoti aje nayo na ikaguliwe).
e) Four figures (mathematical table) moja (1).
f) Mfuko mzuri wa kutosha (school bag) kubebea vifaa vyako isiwe mfuko wa karatasi.
g) Kila mwanafunzi anatakiwa kuleta faili moja (spring file) lililobandikwa picha ndogo (passport size) upande wa kulia juu na picha tatu (3) utakabidhi shuleni.
h) Kitabu cha matokeo

2.4 RATIBA YA SHULE

Wanafunzi wote wanatakiwa kufika shuleni siku zote za masomo saa 1:00 asubuhi na kuondoka saa 9:00 alasiri. Katika ratiba ya shule kuna muda wa kusafisha mazingira, michezo na shughuli za elimu ya kujitegemea (EK), muda wa mafunzo rekebishi na mambo mengine yakupasayo kufanya kama mwanafunzi.

2.5 MASOMO YANAYOFUNDISHWA NI:-

1. Hisabati (Basic Mathematics)
2. Kiswahili
3. Kiingereza (English)
4. Jiografia (Geography)
5. Uraia (Civics)
6. Kemia (Chemistry)
7. Elimu ya viumbe (Biology)
8. Fizikia (Physics)
9. Historia (History)
10. Literature in English (kuanzia kidato cha tatu).

Mbali na masomo hayo darasani, pia kuna vipindi vya kongamano **(Debate**), vilabu vya mahusiano ya jinsia (**FEMA**), **TAKUKURU** na Afya.

NB: sughuli nyingine zinaweza kufanyika baada ya muda wa vipindi vya masomo.

3.0 SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE:

3.1 Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria na. 10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara ya Elimu na mafunzo ya ufundi yenye dhamana ya elimu nchini na ofisi ya Rais TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake baada ya kuripoti shuleni.

a) Heshima kwa viongozi, wazazi na wafanyakazi wote wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
c) Kushiriki kwa makini ufanya maandalio ya jioni (preparation)
d) Kuwahi kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikkamilifu maelezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
g) Kuvaa sare za shule wakati wote unapotakiwa.
h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote na
i) Kutunza mali za umma.

A. HESHIMA

i. Unatakiwa kusimama na kumsalimu Mwalimu au mtu yeyote anayekuzidi umri anapopita, anapoingia darasani au kwenye ukumbi wa mikutano.
ii. Hauruhusiwi kutumia lugha mbaya wakati wowote kati yako na wanafunzi wengine kwa walimu wako na kwa watu wengine.
iii. Unapaswa kuheshimu wafanyakazi wote wa shule kama walezi wako.
iv. Kushirikiana na kusaidiana ni jambo la msingi kwa kila mwanafunzi.
v. Unatakiwa kuthamini na kuheshimu kazi zote.
vi. Hauruhusiwi kabisa kufanya mambo yafuatayo:-
    a) Kuvuta sigara
    b) Kufuga kucha, ndevu na kuwa na nywele zisizowekwa katika hali ya usafi.
    c) Kuvaa mavazi yasiyo ya heshima
    d) Kugombana/kupigana
vii. Unatakiwa kuitika mara moja na kukimbilia alipo anayekuita.

viii. Unatakiwa kuheshimu bendera ya Taifa, picha za viongozi wa serikali, Nembo ya taifa , wimbo wa Taifa na fedha za Taifa.

ix. Unatakiwa kuwa mfano mzuri wa heshima na tabia njema mahali popote unapokuwa.

x. Unatakiwa kunyoosha mkono juu na kusimama unapouliza na kujibu swali.

xi. Unatakiwa kukaa kimya wakati unapokuwa darasani. Usitoke bila ruhusa ya Mwalimu au kiongozi aliyeko darasani.

xii. Unapaswa kutunza mazingira na kuhifadhi miti iliyopandwa.

B. MAHUDHURIO

i. Ni lazima mwanafunzi kuhudhuria muda wote wa masomo.

ii. Unatakiwa kuhudhuria vipindi vyote vya masomo ndani na nje ya darasa.

iii. Unatakiwa kuhudhuria na kushiriki kazi zote za mikono.

iv. Unatakiwa kuhudhuria mikutano ya shule kama baraza la shule, ukaguzi, usafi, kupandisha bendera ya taifa.

C. KUWAHI

i. Unatakiwa kuzoea na kuthamini muda.

ii. Unatakiwa kuwahi katika shughuli zote za shule kama zilivyopangwa katika ratiba ya kila siku.

iii. Unatakiwa kuwahi unaposikia wito wa dharula.

iv. Unatakiwa kufika shuleni wa tarehe zilizopangwa.

D. UVAAJI WA SARE ZA SHULE

Kutakuwa na sare inayojulikana kwa wanafunzi na jumuiya nzima inayokubalika na yenye heshima kitaifa. Sare hiyo itavaliwa wakati wote wa:-

a) Masomo shuleni.
b) Wanafunzi wanapotoka nje ya shule kwa shughuli za shule.
c) Mhadhara wa shule (BARAZA)
d) Wanafunzi wanapokwenda hospitalini, n.k
e) Utavaa nguo za michezo na kuzitumia wakati wa michezo **TU**.
f) Unatakiwa kuwa na vazi la kazi wakati wote wa kazi za mikono.
g) Huruhusiwi kuvaa kofia, viatu vya ghorofa na mapambo mengine.
h) Sare ya shule inatakiwa kuwa safi wakati wote.
i) Unatakiwa kuwa na kitambulisho cha shule unaposafiri au likizo.

E. MIPAKA YA SHULE

i. Huruhusiwi kutoka nje ya mipaka ya shule bila ruhusa maalum.

ii. Huruhusiwi kutembea sehemu zifuatazo isipokuwa kwa kibali maalum:-

a) Chumba cha walimu
b) Ofisi za shule
c) Maabara
d) Nyumba za walimu na wafanyakazi wasio walimu.

iii. Huruhusiwi kutembelea sehemu zifuatazo:-

a) Vilabu vya Pombe
b) Majumba ya starehe
c) Majumba ya kufikia wageni. (Guest house).

MAKOSA MAKUBWA AMBAYO YANAWEZA KUMFUKUZISHA MWANAFUNZI SHULE MARA MOJA

1. Wizi wa aina yoyote ile.
2. Kuoa/ kuolewa
3. Matusi kwa viongozi na watu wanaokuzidi umri na walio chini yako.
4. Ulevi wa Pombe, bangi na madawa ya kulevya.
5. Uasherati
6. Magonjwa ya zinaa
7. Ugomvi ndani na nje ya shule.
8. Kupata/ kusababisha / kutoa mimba.
9. Kosa la jinai lililothibitishwa na mahakama.
10. Kuharibu au kuchana picha za viongozi au Bendera ya Taifa.
11. Kukataa adhabu ya viranja au walimu.
12. Utoro wa aina yoyote ile.

MASHARTI MENGINE

Jaza fomu zifuatazo:-

1. Fomu ya hospitali na kupima afya yako.
2. Fomu ya kukubali sheria za shule.
3. Fomu ya historia ya mwanafunzi

MUHIMU

Ni mategemeo yangu kuwa unaelewa kwamba shule ni mahali pa kujifunzia. Kama unatambua hivyo ndivyo walimu na wanafunzi wenzako ndio nyenzo muhimu kupata mafanikio

…….

CHRISTER .K. KALEGA

MKUU WA SHULE

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA MAFUNZO YA UFUNDI

SHULE YA SEKONDARI IGALUKILO

FOMU YA KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI IGALUKILO

ANUANI YAKO ……
S.L.P 157,
BUSEGA – SIMIYU
TAREHE …….

MKUU WA SHULE,
SHULE YA SEKONDARI IGALUKILO,
S.L.P 330,
BUSEGA
K.K
AFISA MTENDAJI,
KIJIJI CHA ……,
S.L.P 157,
BUSEGA

1. Mimi …… (jina la mwanafunzi) msichana/mvulana nakubali kujiunga na kidato cha …….. katika shule ya sekondari igalukilo – Busega leo tarehe ……. Nitafika shuleni bila kuchelewa. Nitatii sheria za shule na za nchi hii. Nitaishi maisha mazuri, nitakuwa mwanafunzi mwenye bidii na juhudi katika masomo, kazi za nje na michezo.

   JINA LANGU ……..

   SAHIHI YANGU ……

   TAREHE ……

2. Mimi ……. (jina la mzazi/mlezi) nakubali mtoto wangu ……. (jina la mwanafunzi) ajiunge na kusoma katika shule ya sekondari Igalukilo. Ninaahidi kumpatia mwanangu vifaa vyote/ mahitaji yote anayotakiwa kufika nayo shuleni kama ilivyotajwa katika barua ya masharti ya kujiunga na shule hii.

   Nitahakikisha ninafuatilia kwa ukaribu mahudhurio, mwenendo, maendeleo ya mtoto wangu shuleni, na sitasita kumwonya mtoto wangu kutii sheria za shule na kuishi maisha mazuri na kuwa na bidii na juhudi katika masomo na kazi za nje.

   JINA LANGU ……..

   SAHIHI YANGU ……

   TAREHE ……

AHADI YA MZAZI / MLEZI KUKIRI KUKUBALIANA NA SHERIA NA KANUNI ZA SHULE IKIWA NI PAMOJA NA MWANAFUNZI KUTOSHIRIKI KATIKA MIGOMO NA KUTEKELEZA MAELEKEZO MENGINE YATAKAYOTOLEWA NA SHULE

Mimi ……. (jina la mzazi/mlezi) ambaye ni mzazi wa ……. (jina la mwanafunzi) nimesoma na kuelewa vyema maelekezo ya mwanangu kuhusu kujiunga na shule ya sekondari Igalukilo. Hivyo ninakubali kuwa nitasimamia kwa karibu zaidi malezi na maendeleo ya mwanangu kitaaluma na kinidhamu ili asishiriki kwa namna yoyote ile katika migomo ili aweze kumaliza elimu yake ya sekondari vizuri bila kukwama / kukatisha masomo.

“KILA MMOJA ATIMIZE WAJIBU WAKE”

JINA LA MZAZI AU MLEZI ……..……..

SAHIHI ……

TAREHE ……...

NAMBA ZA SIMU ……

KIAMBATISHO A:

OR- TAMISEMI

HALMASHAURI YA WILAYA YA BUSEGA

SHULE YA SEKONDARI IGALUKILO

HISTORIA YA MWANAFUNZI

1. Jina la mwanafunzi ……
2. Shule ya msingi aliyosoma ……
3. Tarehe ya kuzaliwa …….
4. Kabila ……
5. Mkoa …….
6. Wilaya …….
7. Dhehebu/ Dini ……
8. Jina la baba …… (yu hai / kafariki)
9. Jina la mama …… (yu hai / kafariki)
10. Unatoka kijiji cha …… kitongoji …….
11. Kazi ya baba ……
12. Kazi ya mama …….
13. Unaishi na wazazi au walezi? NDIYO/HAPANA
14. Taja jina kamili la mzazi / mlezi ……..
15. Namba za simu za baba …… mama ……. Mlezi ……..
16. Namba ya Cheti cha kuzaliwa ……. (njoo na nakala yake shuleni)

KIAMBATISHO B:

GOVERNMENT OF TANZANIA

REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATIONS

IGALUKILO SECONDARY SCHOOL

PART A:

Full name …….

Age …… Height …… Sex …….. Weight ……

Please examine the above named as to his/ her physical and mental fitness for joining secondary school. The examination should include the following categories (I- III) each category or sub category of which, will render the application ineligible in each of the defect. Pregnancy (Plato test), category IV will render the student ineligible.

I. .

a) Eye sight ……..
b) Hearing ……
c) Speech ……..
d) Venereal disease (HIV) ……..
e) Leprosy and TB disease ……..
f) Epilepsy ……..
g) Spleen ……
h) Chest/Abdomen ……
i) Blood coat …… (red/white)
j) Urinalysis ……

II. Neuroses …….

III. Additional information e.g. physical defect or impairments, infections, chronic or family/ heritable disease (e.g. sickle cell) inability to eat certain food.

……
……
……
……

IV. Pregnancy ……

PART B: MEDICAL CERTIFICATE

(To be completed by a Government medical officer)

I have examined the above named school child and consider that he/she is physically and mentally fit/unfit to attend secondary education course.

Name ……

Signature ……

Designation ……

Station ……